Nuru ya Kiswahili, Juzuu 2(1), Juni 2023: 86 - 112

# Msukumo wa Uwasilishaji wa Hisia za Watoto Kupitia Maigizo ya Utotoni

**Getruda Shima**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

getrudashima2006@yahoo.com

**Ikisiri**
Makala hii inaeleza msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni. Msukumo wa uwasilishaji wa hisia hizo haujawekwa bayana. Hali hii inachangia kutopewa umakini kwa uwasilishaji na uelewekaji wake (Walton, 1990). Nadharia ya Saikolojia Changanuzi, kupitia msingi wa ung'amuzibwete, imetumika kuongoza mjadala wa makala hii. Msingi huo unaeleza kuwa mawazo na matamanio yaliyomo akilini mwa mtunzi wa kazi za kifasihi, hubweteka na kushindwa kutolewa kwa njia ya moja kwa moja kutokana na sababu mbalimbali. Mawazo ya msingi huo yamesaidia kueleza msukumo unaowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Data za utafiti uliozaa makala hii zilipatikana kupitia njia ya mahojiano[1]. Mahojiano yalifanywa kwa wazazi/walezi, walimu wa shule za msingi, wahadhiri wa taaluma za fasihi, na watunzi wa kazi za kifasihi za watoto. Makala inaeleza kuwa sababu za kimchakato-makuzi na kidhima-tanzu huwasukuma watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo tajwa. Makala inapendekeza kuwa wazazi/walezi, walimu na wadau wengine wanaohusika na watoto wasipuuzie maigizo haya kwa kuwa msingi wa uwasilishaji wake ni mchakato wa ukuaji na sifa ya maigizo hayo.

**Dhana za Msingi**: Hisia, Maigizo ya Utotoni, Mtoto, Ung'amuzibwete

[1] Data hizi zilikusanywa na mwandishi wa makala hii mwaka 2019 kwa ajili ya kukamilisha utafiti wa masomo ya ngazi ya uzamivu katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

**Utangulizi**

Dhana *hisia*, ambayo inajitokeza kuwa na maana mbalimbali kwa kuzingatia mwega wa kutumika kwake, katika makala hii inarejelea fikra, hali na matamanio anayokuwa nayo mtunzi wa kazi ya kifasihi kwa kuzingatia muktadha unaohusika. Hivyo, kwa kuwa walengwa wa uwasilishaji wa hisia hizo katika makala hii ni watoto, basi, fikra, hali, na matamanio hayo, ni yale wanayokuwa nayo watoto. Kuhusu *maigizo ya utotoni*, haya ni maigizo wanayoyafanya watoto wenyewe pasipo kupewa maelekezo na watu wazima, na ambayo pia ni sehemu ya michezo yao ya utotoni.

Ufafanuzi wa dhana hizo mbili kwa kuzingatia mwelekeo wa makala hii, umefumbata dhana mtoto. Dhana hiyo ya mtoto inadhaniwa kuwa ni nyepesi katika upatikanaji wa maana yake, lakini ni ngumu kwa kuzingatia miktadha mbalimbali (Bisht, 2008). Dhana mtoto katika uga wa fasihi ya watoto imejadiliwa na wataalam mbalimbali, wakiwamo Bisht (2008), Bajpai (2010), Shima (2012), Bakize (2014), Lyimo (2014), Ngugi (2015), Abdallah (2018), na Mosha (2018). Kigezo cha umri ndicho kilichotamalaki katika mahitimisho ya mjadala kuhusu dhana hiyo ya mtoto. Maafikiano ya kongamano la kimataifa kuhusu haki za mtoto la mwaka 1986 kuwa mtoto ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 yamesaidia kutoa mwongozo kuhusu maana ya dhana mtoto. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwapo kwa marika mbalimbali ya watoto kulingana na wataalamu wa makuzi ya watoto kama vile, Piaget (1953), na, hivyo, kuathiri kazi zinazotungwa na watoto au kwa ajili ya watoto, kunatoa msukumo wa kubainisha rika la watoto waliokusudiwa katika mjadala wa makala hii. Watoto wenye umri wa miaka 5 -11 ndiyo waliokusudiwa katika makala hii. Hii ni kwa sababu watoto

wenye umri huu huwa na uwezo wa kuchangamana na wengine, na hushiriki katika maigizo ya utotoni kwa kiasi kikubwa.

Suala la uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni limezungumzwa kwa namna mbalimbali na wataalamu mbalimbali. Kwa mujibu wa kituo cha *Center on the Social and Emotional Foundations for Early Learning* - CSEFEL (2003), kinachojihusisha na makuzi, pamoja na uhamasishaji wa elimu kwa watoto, huko Florida nchini Marekani, watoto toka kuzaliwa mpaka miaka miwili, hujifunza, kwa kiasi kikubwa, kuhusu mahusiano, hisia, maliwazo, na kujidhibiti. Kituo hicho kinabainisha shughuli na mikakati ya kuwasaidia watoto kuelewa mawazo hayo. Mkakati mmojawapo ni ule unaowahusu watoto wenye umri wa miezi 18 hadi miaka 2, kutumia maigizo ya utotoni kama njia ya kuzungumzia hisia. Wanabainisha kwamba maigizo ya utotoni huweza kuwasilisha hisia mbalimbali kama vile huruma. Maelezo hayo yanadokeza namna maigizo ya utotoni yanavyosaidia uwasilishaji wa hisia za watoto.

Singer na Singer (2005) wanaonesha namna maigizo ya utotoni yalivyo nyenzo muhimu ya kuwasilishia hisia za watoto. Wanabainisha kuwa maigizo hayo huwafanya watoto wawe huru katika kudhihirisha hisia zao ikilinganishwa na uwasilishaji wa kutumia njia nyingine. Hoja hiyo zaidi ya kueleza namna maigizo ya utotoni yalivyo na nafasi muhimu katika kuwasilisha hisia za watoto, vilevile inadokeza kwa namna isiyo ya uwazi kuhusu msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni. Halikadhalika, mawazo yao hayatofautiani sana na ya Fein (1989) na Bretherton (1987) wanaodai kwamba udhibiti wa hisia ni kazi ya msingi ya maigizo ya utotoni. Hivyo, maelezo ya wataalamu hao yanasisitiza uhusiano wa maigizo ya utotoni na hisia. Vilevile, yanashadidia sababu ya

kutumia maigizo ya utotoni ili kueleza msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto.

*Environments Inc* (2003) inabainisha sababu zinazowafanya watoto wacheze michezo mbalimbali, ukiwamo wa maigizo ya utotoni. Sababu hizo ni kujenga mahusiano na watu pamoja na kufanya uvumbuzi unaosaidia kutambua ulimwengu. Vilevile, michezo hiyo ni muhimu katika maendeleo ya mtoto kiumbo, kiakili, kihisia, kijamii na kiubunifu. Maelezo haya yanaonesha umuhimu wa kuchunguza msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni. Sababu zinazowafanya watoto wacheze zinaleta hamasa ya kujua msukumo wa uwasilishaji wa hisia zao kupitia maigizo ya utotoni.

Kwa jumla, uchunguzi kuhusu msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni ulifanywa kutokana na kuwapo kwa mtazamo finyu kuhusu uwasilishaji huo. Mtazamo huo finyu wa wadau mbalimbali kuhusu uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, ulichagizwa na kutojulikana kwa kina kuhusu msukumo unaowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni.

**Kiunzi cha Nadharia**

Nadharia iliyoongoza utafiti ulioibua makala hii ni ya Saikolojia Changanuzi. Nadharia hii iliasisiwa na mwanasaikolojia wa ki-Austria, Sigmund Freud (1856 - 1939). Wahakiki wengine wanaohusishwa na nadharia hii ni Jacques Lacan (1901 - 1981), Carl Jung (1875 - 1961) na Karen Horney (1885 - 1952). Dhana mbalimbali zinazounda Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ni pamoja na ndoto, matamanio ya kingono, na ung'amuzibwete. Ung'amuzibwete hurejelea sehemu ya akili inayohifadhi

fikra na matamanio ambayo mengi ni hasi (Wamitila, 2002; Mushengezi, 2003; Wafula & Njogu, 2007). Mawazo ya ung'amuzibwete ambayo ni msingi mmojawapo wa Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ndiyo yatakayoongoza mjadala wa makala hii. Freud aliamini kuwa kila binadamu huwa na sehemu aliyoieleza kama ung'amuzibwete wa kibinafsi (Wamitila, 2002). Sehemu hii huhifadhi fikra na mawazo mengi hasi yanayobuniwa. Mawazo hayo hayajitokezi waziwazi, bali hujitokeza tu kiishara katika ndoto, utani, sanaa au uandishi, na mitelezo ya kauli. Mawazo na matamanio yanayozungumziwa katika nadharia hii kwa maana nyingine hurejelea hisia ambazo ndiyo mwega wa msingi wa utafiti huu. Kwa kuzingatia sifa za jumla za kundi la watoto, hasa rika la utoto wa kati, ni mwono wa makala hii kuwa hisia hizo zinaweza kuwa na mwegamo chanya pia. Hisia hizo, kwa mujibu wa Nadharia ya Saikolojia Changanuzi hushindwa kutolewa kwa njia ya moja kwa moja kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo vikwazo vya kijamii. Msingi huu unatoa mwongozo wa kujadili msukumo unaowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Maigizo ya utotoni huwapa watoto nafasi ya kubuni na kuwasilisha maigizo hayo.

## Methodolojia

Data za utafiti zilikusanywa katika Mikoa ya Ruvuma na Dar es Salaam. Njia ya mahojiano ndiyo iliyotumika kukusanyia data. Sampuli iliyotumika ilihusisha wazazi/walezi wenye watoto wa rika la kati (miaka 5-11), walimu wa shule za msingi wanaofundisha madarasa ya ngazi za chini (awali - la tatu), watunzi wa kazi za kibunifu za watoto, na wahadhiri wanaofundisha taaluma za fasihi. Watafitiwa waliohojiwa wamepewa msimbo wa namba na herufi, vilivyofuatia hadhi zao kwa kuzingatia nafasi ya kuhojiwa, na eneo la utafiti, mtawalia. Watafitiwa waliohojiwa katika Mkoa wa Ruvuma

wamepewa herufi R, na watafitiwa waliohojiwa katika Mkoa wa Dar es Salaam wamepewa herufi D, isipokuwa kwa wale waliohojiwa katika eneo moja la utafiti, ambao ni watunzi wa kazi za kifasihi za watoto, pamoja na wahadhiri wanaofundisha taaluma za fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Watunzi na wahadhiri hao walihojiwa katika Mkoa wa Dar es Salaam pekee. Kwa hiyo, kundi la wazazi limehusisha Mzazi wa 1R mpaka Mzazi wa 4R, na Mzazi wa 1D mpaka Mzazi wa 4D. Kundi la walimu limehusisha Mwalimu wa 1R mpaka Mwalimu wa 3R, na Mwalimu wa 1D mpaka Mwalimu wa 3D. Kundi la watunzi wa kazi za kifasihi za watoto limehusisha Mtunzi wa 1 mpaka Mtunzi wa 4, na kundi la wahadhiri limehusisha Mhadhiri wa 1 mpaka Mhadhiri wa 5.

**Matokeo ya Utafiti**

Utafiti umebaini kuwapo kwa sababu mbalimbali zinazowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Maelezo kuhusu sababu hizo yanachukuana vema na yale ya msingi wa Nadharia ya Saikolojia Changanuzi kuhusu sababu za uwasilishaji wa fikra na matamanio ya watunzi wa kazi za kifasihi kwa kutumia mbinu za kisanaa. Kwa mujibu wa mawazo ya Nadharia hiyo ya Saikolojia Changanuzi, fikra na matamanio ya watunzi wa kazi za kifasihi hubweteka katika ung'amuzibwete na hushindwa kuyatoa katika hali ya kawaida kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali, zikiwamo za vikwazo vya kijamii, hivyo, kuwafanya wayatoe kwa namna isiyo ya kawaida kama vile mitelezo ya kauli, ndoto, na sanaa.

Utafiti umebaini kuwapo kwa sababu za kimsukumo, yaani zile zinazotoa msukumo kwa watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Sababu hizo ziko katika miegamo miwili. Nayo ni mwegamo wa kimchakato-makuzi na mwegamo wa kidhima-tanzu. Mwegamo wa kwanza

ni ule unaoeleza sababu zinazohusiana na makuzi ya mtoto, na, hivyo, kuibua sababu za kimchakato-makuzi za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni. Mwegamo wa pili ni ule unaoeleza sababu kwa kuzingatia sifa za maigizo ya utotoni, na, hivyo, kuibua sababu za kidhima-tanzu za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni.

**Sababu za Kimchakato-Makuzi**

Sababu za kimchakato-makuzi za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni kutokana na makala hii, ni zile zinazohusiana na makuzi ya mtoto. Sababu hizo ni msukumo wa kimakuzi na vikwazo vya kijamii.

***Msukumo wa Kimakuzi***

Makuzi ya mtoto yameelezwa katika mielekeo tofauti na wataalamu mbalimbali. Mawazo ya uelezaji wao yameibua nadharia mbalimbali zinazozungumzia suala hilo. Miongoni mwazo ni Nadharia ya Ukuaji wa Kiutambuzi ya Jean Piaget (1953), Nadharia ya Mfumo wa Mahitaji ya Maslow (1943), Nadharia ya Ujifunzaji wa Kijamii ya Bandura (1977), na Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ya Freud (1920) kupitia msingi wa ukuaji-kisaikolojia. Mwelekeo wa makala hii inayohusu msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, unaalika ufafanuzi wa Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ya Freud (ameshatajwa) kwa kuwa uwasilishaji huo unajinasibisha na tajiriba mbalimbali ambazo uibukaji wake unamtegemea mtoto, pamoja na wale wanaomkuza. Ekiru (2018) anatoa ufafanuzi kuhusu Nadharia ya Saikolojia Changanuzi kuhusiana na ukuaji wa mtoto kwa kubainisha kuwa akili ya mtoto imegawanyika katika viwango vitatu ambavyo huathiri mabadiliko ya kiutambuzi. Kiwango cha kwanza ni kile cha kimsingi (Id), kinachohusu mambo ya msingi anayoyafanya mtoto kutokana na msukumo wa ndani.

Kiwango cha pili, ni cha kati (Ego), kinachohusu kufikiri na kuona uhalisia wa mambo, na kuyakabili. Kiwango cha tatu, ni cha ukomavu (Super Ego) kinachohusu kujifunza kijamii.

Ufafanuzi kuhusu sifa za mtoto katika kiwango cha tatu kinachohusisha rika la utoto wa kati (miaka 5 - 11) lililolengwa katika makala hii ni pamoja na: kujifunza kupitia vitu mbalimbali katika mazingira yanayomzunguka, kujifunza maadili ya jamii, kuweza kusimulia tukio, na kuwa na uwezo wa kufikiri mambo ya baadaye kwa kuhusisha na ya sasa, na yale yaliyopita. Sifa hizi zinahusiana na kile kinachofanyika katika maigizo ya utotoni. Matundura na wenzake (2013) wanaeleza kuwa miongoni mwa sifa za fasihi ya watoto ni kujihusisha na maudhui ya kukua kwa watoto, na; hivyo, huandikwa kwa mtazamo wa mtoto. Mawazo hayo yanasaidia kuonesha mfungamano uliopo baina ya hatua za mchakato wa makuzi ya watoto na sanaa. Kwa hiyo, maigizo ya utotoni ni njia inayomsaidia mtoto kutimiza azma ya kuwasilisha kile anachokifikiri, kubainisha hali pamoja na matamanio yake kuhusu mambo mbalimbali anayokutana nayo katika jamii. Kwa hiyo, msukumo huo wa kimakuzi humsaidia mtoto kuwasilisha hisia zake kupitia maigizo ya utotoni. Mhadhiri wa 1 kupitia mahojiano anasema:

> Tunaweza tukasema ni hatua mojawapo ya makuzi ya watoto, kwamba kulingana na makuzi, kuna hatua fulani ambazo anapitia. Na inawezekana asipopitia hiyo hatua, ndiyo kuna watu utakuta wanasema fulani aliruka ‘stage’ (ikiwa na maana ya hatua. TY) ndiyo maana anafanya mambo ambayo si ya ‘stage’ yake. Na vile vitu nafikiri ni kama asili, yaani vipo. Hata mtoto umfungie ndani, kuna mambo tu ambayo atayafanya huko. Kuna matendo ambayo atayafanya hata awe peke yake, na anavyofanya, atakuwa kama yupo na wenzake kumi hivi.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Maelezo hayo ya Mhadhiri wa 1 yanasisitiza kuhusu sababu za uwasilishaji wa hisia za watoto kuwa ni kutokana na msukumo wa kimakuzi. Maelezo yake yanabainisha kuwa zipo hatua mbalimbali za makuzi ambazo mtoto anazipitia, na uigizaji unakuwa ni miongoni mwa mambo anayopaswa kuyafanya mtoto ili kuendana na hatua hizo za kimakuzi. Hii inamaanisha kuwa msukumo huo wa kimakuzi huwa ni wa asili. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine, mtoto hupitia maigizo ya utotoni kama inavyoelezwa pia na Mwalimu wa 1R kupitia mahojiano. Mwalimu huyo anaeleza kuwa "kwa namna nyingine huwa ni kama vile Mungu amewapa upendeleo au karama ya kuwasilisha hisia zao kupitia matendo mbalimbali, yakiwemo maigizo ya utotoni." Dondoo hilo linahusiana na sehemu ya maelezo ya Mhadhiri 1 kama ilivyokwishabainishwa.

Msingi wa maelezo hayo ni kuonesha kuwa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni huchochewa na msukumo wa kimakuzi. Msukumo huo unatanababahisha kuhusu kuwapo kwa hatua mbalimbali za makuzi ya watoto. Sifa za kila hatua, huwapa watoto nafasi ya kuchangamana na wengine. Suala hili linapewa mkazo na Sheridan (2002) anayebainisha kuwa ukuaji wa mtoto huwa hauishii katika uongezekaji na ukomavu wa viungo vya mwili tu, bali pia huhusu upataji wa maarifa mbalimbali yenye manufaa kwa mtoto. Kupitia michezo yao mbalimbali, ambapo maigizo ya utotoni ni miongoni mwa hiyo, watoto hueleza fikra, mitazamo, na matamanio yao. Miongoni mwa sifa zinazotamalaki kwa rika la utoto wa kati, kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu wa makuzi ya mtoto, ni athari ya mazingira kuhusiana na utambuzi wa mambo mbalimbali. Hivyo, mazingira yana nafasi muhimu katika kutoa msukumo wa watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni.

Maelezo kuhusu nafasi ya mazingira kuwa miongoni mwa mambo yanayowasukuma watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni, yakilenga sababu za msukumo wa kimakuzi yanatolewa na Mhadhiri wa 4. Mhadhiri huyo anabainisha kuwa nadharia mbalimbali zinazoeleza jinsi watoto wanavyojifunza na kutambua vitu katika hatua za utoto wa awali zinaonesha athari ya mazingira katika kukamilisha mchakato huo. Maigizo ya utotoni huakisi utamaduni wa jamii inayowazunguka watoto (Gosso na Carvalho, 2013). Kutokana na maelezo hayo, sababu za msukumo wa kimakuzi zinazowachochea watoto kuwasilisha hisia zao, haziwezi kujitenga na mazingira au jamii ambayo humkuza mtoto.

Kwa hiyo, msukumo wa kimakuzi huwachochea watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Hali hii ndiyo inayosababisha watoto wengi, kwa kujua au kutokujua, kutenda maigizo ya utotoni na kuyafanya ni sehemu ya michezo yao ya utotoni. Uigizaji wa mtoto huwa ni njia ya kujifunza mambo mbalimbali anayokutana nayo katika jamii. Vilevile, ni namna ya kuyaweka katika vitendo mambo mbalimbali aliyojifunza kutoka katika jamii. Msukumo wa kimakuzi husababisha fikra, hali, na matamanio ya mtoto kuwekwa bayana kupitia maigizo ya utotoni. Hivyo, kwa kuzingatia maelezo ya Nadharia ya Saikolojia Changanuzi kuhusu kuwapo kwa sababu za uwasilishaji wa mawazo ya mtunzi wa kazi za kifasihi, msukumo wa kimakuzi huwapa watoto nafasi ya kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Ridhiko la mtoto kupitia hisia zake linajitokeza kuwa na nafasi ya kumkuza katika njia ipasayo, na, hivyo, kuondoa migogoro ya kijamii. Mawazo haya kuhusu hoja ya msukumo wa kimakuzi kuwa sababu ya uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni yanaungana na ya wataalam Nespeca na Reeve (2003) wanaosema kwamba

kila mmoja wetu, kwa kujua au kutokujua, amepitia utendaji wa maigizo ya utotoni. Pia, yanashadidiwa kuwa maigizo ya utotoni ni sanaa ya mwanzo kutendwa na binadamu. Hivyo, utendaji wake si wa bahati mbaya, bali hutokana na msukumo wa kimakuzi.

Msukumo wa kimakuzi pia huchangamana na utegemezi. Tangu kuzaliwa kwake, mtoto huishi katika kumtegemea au kuwategemea wazazi au walezi wake katika kutimiza mahitaji yake ya msingi na ya ziada (Mahan, 1969). Kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujitimizia mahitaji hayo, mtoto hulazimika kuishi kwa kuwategemea wazazi au walezi mpaka pale atakapoanza kujitegemea (Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, 2014). Kwa hiyo, upatikanaji wa hitaji fulani, liwe limeombwa au halikuombwa, hutegemea uwezo na matakwa ya wazazi au walezi wake.

Hali hiyo ya utegemezi huwasukuma watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Hii ni kwa sababu, mtoto hutafuta kujitimizia au kueleza kuhusu mahitaji yake au jambo lolote kwa namna nyingine ambayo itamfanya aweze kumiliki au kuelezea hitaji fulani ingawa si kwa uhalisia. Hueleza fikra, hali na matamanio yake kupitia maigizo ya utotoni kutokana na maigizo hayo kutomuwekea mipaka, na, hivyo, kuibua uhalisi wa kibunilizi. Mzazi wa 2D, Mzazi wa 3R, na Mwalimu 1D wanatoa maelezo yanayolingana kuhusu namna utegemezi unavyochangia uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni kwa kuzingatia suala la kimahusiano kati ya watoto na wale wanaowategemea. Kwa mfano, Mzazi wa 2D katika mahojiano anasema:

> Hisia hizo za watoto huwasilishwa kwa sababu maalumu. Kwa mfano, mtoto anapotengeneza boksi kama luninga na kuliweka ndani, huonyesha hisia zake za kuhitaji kitu hicho. Hali hiyo hutokea kwa sababu mtoto huwa katika utegemezi wa mahitaji yake yote. Kwa hiyo, kama mzazi, baada ya kuliona hilo, ni jukumu langu kupambana ili niweze kununua kitu hicho. Kwa hiyo, anakuwa amesaidia kunikumbusha kama nilikuwa nimelala. Kwa hiyo, malaika anakuwa amekukumbusha kwa njia ya maigizo na hisia.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Maelezo ya dondoo hilo yanaonesha kuwa suala la utegemezi huwafanya watoto washindwe kupata mahitaji wanayofikiri kuyapata. Badala yake, hudumu katika matamanio, na, hatimaye, kuyawasilisha matamanio ya mahitaji na hali mbalimbali kupitia maigizo ya utotoni kwa kuzingatia uhuru wa utendaji wake. Huko 'New Orleans' mji upatikanao Jimbo la Louisiana nchini Marekani, huendeshwa mashindano ya kutambaa kwa watoto wadogo. Watoto hao ni wale walio katika rika la kutambaa. Matamanio ya wazazi wenye watoto wanaoshiriki shindano husika huwa ni kuona watoto wao wanapata ushindi. Inapopigwa filimbi kwa ajili ya kuanza shindano, watoto wengine huwang'ang'ania wazazi wao kwa kutotaka kushuka ili kuanza mashindano, wengine hutambaa kidogo na kukaa, wengine huanza kucheza wao kwa wao katikati ya uwanja, wengine hutambaa na kufika karibu na mwisho, lakini, ghafla, hugeuka na kurudi walikotoka, na wengine husimama na kutembea badala ya kutambaa, hivyo, kuvunja kanuni za shindano hilo. Ijapokuwa ni vigumu kwa watoto kuelewa kinachoendelea katika mashindano hayo, kutokana na umri wao, hata hivyo, wazazi hutarajia ushindi kutoka kwa watoto wao. Kwa hiyo, huwa hawana namna, zaidi ya kuwavutia watoto kwa vitu mbalimbali, ilimradi tu waweze kufika mwisho, na, hivyo, kuibuka na ushindi.

Ili kuyafanya matamanio ya watoto yawe katika uhalisi, kwa mujibu wa makala hii, ni suala linalohitaji umakini wa wazazi, walezi pamoja na jamii inayomzunguka mtoto. Vinginevyo, ridhiko la mtoto huyo litaishia katika maigizo hayo tu.Vilevile, yale anayoyawasilisha mtoto, kwa maana ya hisia zake, hutegemea yale yanayodhihirishwa na wazazi au walezi. Yaani, mambo anayoyawasilisha mtoto, huakisi yale yanayotolewa na mtegemezi wake. Kwa hiyo, tabia, mienendo, pamoja na mwonekano wa wanajamii wanaotangamana na mtoto vina athari katika uwasilishaji wa hisia za mtoto, na, kwa mantiki hiyo, vinajitokeza kuwa sababu ya uwasilishaji wa hisia hizo za watoto kupitia maigizo ya utotoni.

***Vikwazo vya Kijamii***

Utafiti unaonesha kuwa vikwazo vya kijamii ni miongoni mwa sababu zinazowasukuma watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Hoja hii imejengewa msingi wake na mawazo ya Nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Kwa mujibu wa mawazo ya nadharia hii, kupitia msingi wa ung’amuzibwete, fikra na matamanio anayokuwa nayo mtunzi wa kazi ya fasihi hubanwa au kuhifadhiwa katika sehemu ya ubongo ya ung’amuzibwete, na kushindwa kwake kutolewa husababishwa na mambo mbalimbali, likiwamo la vikwazo au mikatale ya kijamii. Matokeo yake, hutolewa kwa namna nyingine isiyo ya moja kwa moja, kwa mfano ndoto, sanaa na mitelezo ya kauli.

Imebainika kuwa vikwazo vya kijamii vinasababishwa na mambo mbalimbali, na miongoni mwavyo ni ukali na fikra potofu kuhusu kundi la watoto. Kuhusu hoja ya ukali, wazazi wanapokuwa wakali kwa watoto, huwa kikwazo kwa watoto hao kuwasilisha hisia zao kupitia njia za kawaida. Ukali hujenga hofu na wasiwasi kwa watoto kiasi cha kujenga uadui usio bayana baina yao. Na kutokana na kutoepukika kwa suala la

hisia kwa watoto, hujikuta wakizitoa kwa namna nyingine inayowapa uhuru wa kufanya hivyo. Maigizo ya utotoni ni njia mojawapo inayomfanya mtoto awe huru katika mambo mbalimbali. Kwa mfano, kufikiri/kuanzisha wazo, kubuni njia za kuliwasilisha, na, hatimaye, kuwasilisha yale yote anayosukumwa nayo. Mwalimu wa 3R kupitia mahojiano anasema:

> ... Ni kutokana na jinsi mazingira tuliyokuwa nayo. Unaweza kukuta mwalimu anakuwa mkali sana na hivyo mtoto kumtamkia moja kwa moja kuwa labda nikimaliza masomo nataka kufanya kazi fulani inakuwa vigumu. Kingine, wale watoto wapo katika mazingira ya utoto, kwa hiyo hata ubongo wao unahisia tu. Wanatamani kufanya vitu, lakini umri wao pia unawavutia nyuma kwa hiyo wanaona bora waonyeshe kwa njia ya hisia kuliko kutamka moja kwa moja. Hujijengea mawazo kuwa "kwa umri huu mimi sitaweza." Na sababu nyingine ni kuwa, wazazi, hata jamii kwa ujumla inaweza kuwakatisha tamaa. Mtoto hana sauti mbele ya wazazi au jamii. Hukatishwa tamaa na jamii husika.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Maelezo hayo yanaonesha namna vikwazo vya kijamii vinavyohusu ukali wa wazazi au walezi vinavyochochea uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni. Kutokana na hoja hii, swali linaweza kuibuka kwamba, iwapo wazazi wataacha au kuondokana na hali ya ukali kwa watoto wao, hivyo kuwafanya watoto hao wawasilishe hisia zao katika hali ya kawaida, ina maana hapatakuwa na haja ya maigizo ya utotoni kutumika katika kuwasilisha hisia za watoto? Kwa kuzingatia kuwa uchunguzi uliozaa makala hii ulihusisha maigizo ya utotoni, kwa hiyo, sentensi ya pili kutoka mwisho wa dondoo hilo inayosema, "mtoto hana sauti mbele ya wazazi au jamii," inapohusishwa na madhumuni ya makala, inatoa jibu kuwa, athari za ukali wa wazazi kwa watoto katika mazingira halisi, hutoa

msukumo kwa watoto kuwasilisha hisia kuhusu hali hiyo katika maigizo ya utotoni. Akizungumzia namna ukali usivyokuwa njia pekee ya malezi, Ndossa (2019) anayataja madhara ya ukali katika malezi ya watoto kuwa ni pamoja na: nidhamu ya woga, huondoa kujiamini, hofu na kushindwa kujieleza, pamoja na kupunguza mapenzi. Anatoa ufafanuzi kuhusu suala la hofu na kushindwa kujieleza kwa watoto kutokana na ukali wa wazazi kwa kusema:

> Malezi ya ukali huwafanya watoto kuogopa kuripoti matukio ya hatari. Kama kuna hatari kubwa kwa watoto wetu katika zama hizi, basi ni kule kushindwa kwao kuripoti matukio ya hatari. Hii ni kutokana na ukweli kuwa watoto wamejengewa hofu na wazazi wao kiasi cha kushindwa kuwakimbilia katika matatizo. Hali hii inathibitishwa na namna matukio mengi ya kudhalilisha watoto yamekuwa yakichukua muda mrefu kubainika.

Hapo, Ndossa (*keshatajwa*) anaonesha namna suala la ukali katika malezi ya watoto linavyosababisha watoto washindwe kujieleza kwa uhuru. Kutokana na ukali huo, kwa mujibu wa makala hii, watoto hutafuta namna nyingine ya kuwasilisha hisia zao, ambayo ni kutumia maigizo ya utotoni. Maelezo hayo kuhusu sababu za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni kwa kuzingatia ukali wa wazazi kama kikwazo cha kijamii, yanahusiana na vikwazo vya kijamii vya fikra potofu kuhusu kundi la watoto na maigizo ya utotoni ingawa si kwa muumano wa moja kwa moja. Akizungumzia kuhusu hoja hii ya vikwazo vya kijamii kuhusiana na fikra potofu kuhusu kundi la watoto na maigizo ya utotoni, Mzazi wa 3D anabainisha kuwa:

> Mtoto mwingine anaweza kufanya maigizo ya utotoni, mzazi anamkataza. Kumbe anavyomkataza, anamharibia. Wazungu humuacha. Sisi Waafrika huwa tunawakaripia ... Tuwape muda watoto wanapokuwa nyumbani ili wapate kucheza michezo yao ile ya asili.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Vikwazo hivyo vya kijamii kuhusu fikra potofu kwa watoto pamoja na maigizo ya utotoni, kama ilivyobainishwa, hutoa msukumo kwa watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Kwa kuwa uwasilishaji wa hisia hizo huwa haujitengi na jamii, inawezekana hata mawazo hayo potofu ya wazazi au walezi yakaweza kudhihirishwa kupitia maigizo hayo ya utotoni. Hivyo basi, mawazo hasi ya wazazi kwa watoto, huzaa mawazo hasi ya watoto kwa wazazi.

**Sababu za Kidhima-tanzu**

Sababu za kidhima-tanzu za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, kutokana na utafiti uliofanyika, kama ilivyobainishwa hapo awali, zimejiegemeza katika dhima za utanzu wa maigizo ya utotoni. Kwa kuwa watoto wengi hupata ugumu kutambua wazi na hata kueleza hisia zao kuhusiana na hali wanazozipitia, hadithi huweza kutumika kama kisaidizi cha majadiliano na ujitambulishaji (Ngugi, 2015). Kwa kuzingatia mawazo hayo ya Ngugi (*keshatajwa*), maigizo ya utotoni yamejitokeza kuwa na sifa zinazowasukuma watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Dhima za maigizo hayo ya utotoni, kulingana na makala hii, ni pamoja na: kuwafanya watoto wajitenge na ulimwengu halisi, na kuwafanya waweze kutangamana.

***Kujitenga na Ulimwengu Halisi***

Watoto huwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni kwa kuwa maigizo hayo huwatenga na ulimwengu halisi. Wakizungumzia kuhusu dhana ya

ulimwengu wa kifasihi, Ngugi na wenzake (2019) wanasema, “kimsingi, kazi ya fasihi huwa na ulimwengu wake ambao unajengwa na mwandishi.” Maelezo hayo yanashadidia kuwapo kwa kanuni na kaida za kifasihi zinazotawala ulimwengu huo. Wanapotenda maigizo ya utotoni, watoto huumba ulimwengu wa kibunilizi ndani ya ulimwengu halisi. Ulimwengu huo wa kibunilizi huwaruhusu kuwasilisha hisia zao pasi na mwingilio wa kijamii. Hii huwafanya waweze kueleza fikra zao, hali zao, pamoja na matamanio ya kihalisia kwa uhuru, bila woga wowote. Ulimwengu wa kibunilizi huwaruhusu kutenda, kuzungumza, kutumia vifaa mbalimbali, pamoja na kuuvaa uhusika unaodokeza uhalisia kwa kutumia ubunilizi. Ingawa mambo hayo huyatenda ndani ya uhalisi, lakini ubunilizi hufunika macho yao kiasi cha kuwafanya wasiuone uhalisi na mambo yaliyomo katika uhalisi huo.

Kwa upande mwingine, ulimwengu huo wa kibunilizi huifanya jamii kutoingilia kile kinachofanyika, hivyo, kuzidi kulipa nafasi suala la uhuru wa kimawazo na utendaji wa maigizo hayo. Mawazo hayo yana msingi wake katika Nadharia ya Saikolojia Changanuzi kuwa mawazo na matamanio anayokuwa nayo mtunzi wa kazi ya kifasihi hubweteka katika ung’amuzibwete kutokana na sababu mbalimbali, na, hatimaye, hutolewa kwa njia ya kisanaa. Hii ina maana kwamba sanaa ya fasihi humfanya mtunzi kuwa huru katika kuwasilisha yale aliyokusudia. Hivyo, maigizo ya utotoni humfanya mtoto ajitenge na ulimwengu halisi, na hatimaye, kuwasilisha hisia zake pasipo na mwingilio. Katika kuelezea hoja ya kujitenga huko ikiwa ni sababu inayowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni, Mtunzi wa 2 anatoa mawazo ya jumla yanayogusia suala la kujitenga na ulimwengu halisi linavyojitokeza kuwa ni

sababu inayowafanya watoto wawasilishe hisia zao kupitia maigizo ya utotoni. Mtafitiwa huyo aliyatoa mawazo hayo kupitia mfano wa mtunzi wa kazi za kifasihi zinazowalenga watoto kwa kuzingatia nafasi yake pamoja na uzoefu alio nao. Kinachosisitizwa na Mtunzi wa 2 ni namna maigizo ya utotoni yanavyomfanya mtoto awe huru kuwasilisha hisia zake zinazohusu mambo halisi kupitia ubunilizi unaotimilizwa na kule kujitenga na ulimwengu halisi. Nao wahadhiri wa 2 na 4 wanaongeza maelezo kuhusu suala la kujitenga na ulimwengu halisi na uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni kuwa matendo, vifaa, mandhari, pamoja na majina ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kujitenga huko na ulimwengu halisi ingawa huwa hakuachani na jamii.

Suala la kujitenga na ulimwengu halisi lina mchango wa kuwa kisababishi cha uwasilishaji wa hisia mbalimbali za watoto. Ni kupitia kujitenga huko kunakoukiliwa na vipengele vya vifaa, mandhari, majina, pamoja na matendo mbalimbali, watoto huupata uhuru wa uwasilishaji wa fikra, hali na matamanio waliyonayo kwa kuzingatia uhalisi wa kijamii. Watoto kupitia kwa michezo hii hupata fursa ya kumithili nafsi mbalimbali katika ulimwengu wao dhanifu (Ojiambo, 2004). Hii inaonesha ni kwa namna gani watoto hupata nafasi nzuri ya kuwasilisha hisia zao katika ulimwengu wa kibunilizi wa maigizo ya utotoni. Kupitia matendo mbalimbali wanayoyafanya watoto katika maigizo hayo kama vile kupika, kuvua, na kuchunga, hisia za fikra, hali na matamanio huwasilishwa.

***Kutangamana***

Kutangamana ni kitendo cha kushirikiana kwa watu katika jamii. Kwa hiyo, kutangamana ni kitendo cha kujiweka kwenye kundi au kuwa miongoni mwa watu wengine, hivyo, kuondokana na hali ya upweke. Mtoto

anapofikia umri fulani, hususani rika la utoto wa kati katika ukuaji wake, ule ukaribu aliokuwa nao awali kwa wazazi au walezi wake huanza kumwondoka, na, hivyo, kumjengea hali ya kutangamana na wenzake. Michezo mbalimbali ni miongoni mwa mambo yanayochangia kumsukuma mtoto kutangamana na wenzake (*Environmental Inc*, 2003). Kumudu lugha pia huchochea hali hiyo ya kutangamana. Maigizo ya utotoni yakiwa ni sehemu ya michezo ya watoto humsaidia mtoto kutangamana na wenzake. Uhusika na majukumu anayoyabeba mtoto katika maigizo hayo humfanya awe katika mahusiano na wahusika wengine. Huweza kushiriki katika utoaji wa wazo la igizo, utoaji maagizo na upokeaji maagizo kuhusu utekelezaji wa jukumu fulani, pamoja na kuwa katika mazungumzo mbalimbali. Kuhusu suala hili la kutangamana kwa watoto kutokana na maigizo ya utotoni, na, hivyo, kusaidia uwasilishaji wa hisia za watoto, Mwalimu wa 1R anasema:

> Kwenye maigizo haya, watoto hawa mara nyingi huwa wanakuwa na dhana moja wanayofanya. Wanapoyafanya maigizo haya kwa pamoja kunawasaidia kukumbushana mambo mengine ambayo pengine mwingine aliyasahau, lakini labda yalimletea madhara au labda yalimfurahisha. Wanajaribu kujijengea uwezo wao wa kufanya matendo ambayo yanalingana na umri wao. Kwa mfano, wanapojifunza kupika vile vyakula vyao kwenye makopo, wanaashiria kwamba watakapokuwa watu wazima, na wenyewe watafanya hiki kitu. Pale inakuwa kama ni mafunzo ya mwanzo, ama darasa la mwanzo kwao.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Kutangamana huko kunapomwondolea mtoto upweke humsaidia kuwasilisha hisia zake kwa namna mbalimbali. Kwanza, kunamfanya awe huru kwa kuwa, mara nyingi, kundi analokuwa nalo huwa ni la rika lake. Pili, kunamsaidia kukumbuka mambo mbalimbali kutokana na kuangalia

yanayofanywa na wengine, na, hivyo, kumwongezea mambo anuwai yenye kuchochea uibukaji wa hisia. Tatu, kunampa hamasa ya kuwa na fikra changamani, yaani hisia za namna mbalimbali. Na nne, kunamjengea hali ya ulinganishi, na, hivyo, kuchochea hisia zinazotolewa. Hii humsaidia kutoa fikra zake kuhusu mambo mbalimbali, kuonesha hali alizonazo, pamoja na matamanio yake.

Suala la kutangamana pia huchochea fikra za watoto. Fikra wanazozipata watoto kupitia maigizo ya utotoni huanzia kwenye wazo la igizo. Kwa kawaida, hapawezi kuwapo na igizo la utotoni ambalo halina suala linalowasilishwa. Msingi wake hutoka katika wazo ambalo mtoto analiwasilisha. Kutofautiana kwa mawazo ya uigizaji ni ishara kuwa hisia zinazowasilishwa na watoto hazifanani, na, hivyo, uwasilishwaji wake hutegemea mguso wa mtoto husika. Zaidi ya wazo la igizo kuchochea fikra za mtoto, mambo mengine yanayochochea fikra zake na kuwa sababu ya uwasilishaji wa hisia zake ni pamoja na wahusika, mtiririko wa matukio na uumbaji wa mandhari. Haya yote huifanya akili ya mtoto ijikite katika kufikiria mambo mbalimbali na kumjengea kumbukumbu kuhusu hisia tofauti. Mawazo ya Mzazi wa 3D yanashadidia suala la ufikirishi unaotokana na maigizo ya utotoni kuchochea uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni kama ifuatavyo:

> Mimi kwanza huwa napenda, kwa sababu mtoto anapocheza michezo ile huwa ametulia. Akili yake yote huwa inakuwa ipo pale. Akikaa hapo na asiwe na mtu wa kumvurugavuruga huwa anatulia sana. Kwa hiyo, anaweza kuonyesha mengi sana kupitia yale maigizo.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Utulivu wa akili ya mtoto wakati wa utendaji wa maigizo ya utotoni kama ulivyobainishwa na dondoo hilo, humjengea mtoto hali ya kufikiri kuhusu

mambo mbalimbali anayokusudia kuyafanya katika maigizo hayo. Utulivu huo humpa nafasi ya kufikiria kuhusu matukio, wahusika na mahusiano yao, miktadha mbalimbali, pamoja na matendo ya kuyafanya ambayo huwa ni nadra kwayo kupingana na uhalisia, na, kwa mantiki hiyo, hisia za fikra, hali na matamanio huwasilishwa. Maelezo ya Mzazi wa 3D, kama yalivyobainishwa, yanalingana na yale ya Mwalimu wa 3R anayesema kwamba "maigizo ya utotoni hupanua akili ya watoto na kuwafanya wafikiri mambo mengi sana." Ingawa mambo hayo wanayoyafikiri hujikita katika ubunilizi kwa kuzingatia maigizo hayo ya utotoni, hata hivyo, kwa kuzingatia suala la ufungamani wa sanaa na jamii, uhalisi wa kisanaa hujipambanua kupitia mambo hayo, na, hivyo, kuibua uwasilishaji wa hisia za watoto.

Vilevile, ufikirishi, ikiwa ni dhima mojawapo ya maigizo ya utotoni, na uliobainishwa na makala hii kuwa ni jambo linalowachochea watoto kuwasilisha hisia zao kupitia maigizo ya utotoni, limeelezwa kwa namna nyingine na Mtunzi wa 3 kuwa:

> Nakumbuka nilikuwa Mwanza natengeneza video ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Ilihusisha watoto wa shule mbalimbali za msingi. Sasa, kukawa na sehemu ya wimbo ambao ulikuwa unahuzunisha kwelikweli. Ulikuwa unaitwa "Watoto Tunalia". Nikawaambia watoto wakifika sehemu hiyo ya maneno tunalia waigize kulia. Huwezi kuamini, mpaka mimi mwenyewe nilikuwa najisikia vibaya, yaani watoto walilia kiukweli kabisa. Ndiyo, ni kuigiza, lakini kwa wakati ule mpaka mimi mwenyewe kilinigusa na nikajiuliza ni kwa nini watoto wanalia namna ile, yaani kwa hisia za ndani kabisa. Na kuna wakati nilikuwa siangalii kabisa kwa sababu nilihofia kuanza kulia na mimi.
> **Chanzo**: Utafiti (2019)

Kupitia vipengele mbalimbali vya kibunilizi, kama ilivyobainishwa na dondoo hilo, watoto hujenga fikra ambazo kwazo hisia mbalimbali huwasilishwa kutegemeana na yale yaliyobebwa na vipengele hivyo. Kwa mfano, kupitia uimbaji wa wimbo uliobainishwa, watoto waliigiza matendo mbalimbali kama vile kulia na kuwa katika hali ya huzuni. Ni kutokana na uigaji huo uliopewa msukumo na kipengele cha wimbo uliokuwa na mawazo ya kuhuzunisha, watoto walijenga fikra kwa kuzingatia miktadha mbalimbali ya kihalisia, na, hivyo, kuwasilisha hisia za hali ya huzuni iliyoathiri watazamaji na wasilikizaji wake. Ndiyo kusema kuwa ufikirishi utokanao na dhima za kihusika katika maigizo ya utotoni huzalisha uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni.

Kulingana na maelezo yaliyowasilishwa kuhusu sababu za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, imebainika kuwa, katika maigizo ya utotoni, watoto, kwa kiasi kikubwa, huwasilisha hisia zao pasipo wenyewe kujua kuwa wanafanya hivyo. Hali hii inachagizwa na sifa za kimakuzi, pamoja na utanzu unaohusika. Katika ukuaji wake, mtoto hupata msukumo wa kutambua vitu na mambo mbalimbali. Kupitia milango ya fahamu ambayo ni macho, masikio, pua, mdomo, na ngozi, mtoto huuelewa ulimwengu kupitia kuona, kusikia, kunusa, kuonja, na kuhisi. Vilevile, kwa kuzingatia muktadha wa kuzaliwa na kukuzwa kwake, mtoto hufumbatwa na jamii ambayo pia ina mchango mkubwa katika kumtambulisha vitu na mambo mbalimbali yaliyomo humo. Kufumbatwa huko kwa mtoto katika jamii yake, humweka katika hali ya utegemezi wa kimahitaji na kimawazo. Hali hiyo ya kiutegemezi huibua vikwazo vya kimtazamo kuhusu tajiriba za kijamii kuhusiana na mtoto, na, hivyo, kuzuia ujitokezaji wa kimtazamo wa tambuzi mbalimbali ambazo huzaa hisia kwa

mujibu wa makala hii. Hali hiyo ya mtoto kuwa na mawazo, fikra, na matamanio ya kilimwengu imeelezwa pia na Ngugi (2014:171) kuwa:

> Kuna matakwa ya kilimwengu ambayo mtoto anahitaji kujifunza na kuyatekeleza kuanzia kwa kuwa na misimamo yake hadi kuipokea au kuikataa misimamo ya makundi rika. Vilevile, kuna matakwa ya ndani ambayo mtoto anahitaji kuyatekeleza. Kwa mfano, kujua namna ya kudhibiti hasira zake na namna ya kukabiliana na njaa. Ama akiweza kukabiliana na matakwa haya kwa njia maalumu, basi itachukuliwa kuwa anaanza kuuelewa ulimwengu wake wa ndani na nje. Fasihi inaweza kuchangia katika kumsaidia mtoto kukubali hali fulani na hata kujua namna ya kukabiliana na hali nyinginezo ambazo zitaendelea kuibuka katika maisha yake kila kukicha.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Saikolojia Changanuzi, upapatuzi huo wa kimfumbato huishia kutia nanga katika maigizo ya utotoni kutokana na sifa zake za kitanzu. Kwa mujibu wa maelezo ya nadharia hiyo ya Saikolojia Changanunzi, mawazo, fikra, na matamanio anayokuwa nayo mtunzi wa kazi ya kifasihi hubweteka katika sehemu ya ung'amuzibwete na hujitokeza baadaye kupitia njia mbalimbali, ikiwamo sanaa. Matundura na wenzake (2013) wanasisitiza nafasi ya sanaa katika uibuaji wa hisia za watoto kwa kusema kwamba "Fasihi ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira ya nyumbani, jamii zao na ulimwengu kwa ujumla." Hivyo, watoto hutumia maigizo ya utotoni yakiwa ni njia ya kuwasilishia yale yaliyo katika akili yao na kwa kuzingatia muktadha husika. Maigizo hayo humwezesha mtoto kujitenga na mazingira halisi. Hali hii humwezesha mtoto kuuelezea uhalisi kwa namna isiyo ya moja kwa moja. Vilevile, hali ya kutangamana husaidia kuzalisha hisia za namna mbalimbali. Halikadhalika, ufikirishi huchochea uibukaji wa hisia kupitia vipengele mbalimbali kama vile matukio na wahusika.

**Hitimisho**

Kulingana na mjadala wa makala hii, msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni umejitokeza kuangukia katika makundi makubwa mawili. Kundi la kwanza ni msukumo unaohusiana na mchakato wa kimakuzi wa watoto, ambao unaibua sababu za kimchakato-makuzi. Sababu hizo za kimchakato-makuzi ni pamoja na msukumo wa kimakuzi na vikwazo vya kijamii. Msukumo unaoangukia kundi la pili ni ule unaohusiana na dhima ya tanzu ya maigizo ya utotoni, uliosaidia kuibua sababu za kidhima-tanzu za uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia tanzu ya maigizo ya utotoni. Sababu hizo za kidhima-tanzu zilizoelezwa ni kujitenga na ulimwengu halisi, na kutangamana. Kwa hiyo, mjadala huo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni una nafasi ya kuyapa tija maigizo ya utotoni pamoja na hisia zinazowasilishwa. Hii ina maana kuwa, uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, huukiliwa na sababu mbalimbali kama zilivyobainishwa katika makala hii. Hii ni kama inavyojitokeza katika kazi nyingine za kifasihi au pengine tanzu nyingine za fasihi ya watoto. Tofauti yake na uwasilishaji wa namna nyingine katika sanaa nyingine ni katika upekee wa utanzu wa maigizo ya utotoni. Maigizo haya huwashirikisha watoto katika mchakato wa uwasilishwaji wake, yaani utunzi na uwasilishaji. Msukumo wa uwasilishaji wa hisia za watoto kupitia maigizo ya utotoni, kama ulivyobainishwa na makala hii, unachangia upewaji umakini wa maigizo ya utotoni pamoja na hisia zinazowasilishwa kwa manufaa ya watoto na jamii kwa ujumla.

**Marejeleo**

(CSEFEL), T. C. on the S. and E. F. for E. L. (2003). *Teaching your Child About Feelings: From Birth to Age 2*. Vanderbilt. Imesomwa kutoka, Vanderbilt.edu/csefel.

Abdallah, S. (2018). Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika kukuza Fasihi Simulizi: Mifano kutoka katika Vibonzo Jongevu (Tasinifu ya uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bajpai, A. (2010). *The Legislative and Institutional Framework for Protection of Children in India* (IHD - UNICEF Working Paper Series Children of India: Rights and Opportunities No. Working Paper No. 5 The). New Delhi.

Bandura, A. (1977). *Social Learning Theory*. Englewood Cliffs, NJ: Prentice Hall.

Bisht, R. (2008). Who is A Child?: The Adults' Perspective within Adult-Child Relationship in India. *Interpersona: An International Journal on Personal Relationships*, 2 (2), 151 - 172. https://doi.org/10.5964/ijpr.v2i2.24.

Bretherton, P. (1987). Pretense: The Form and Function of Make-believe Play. In *Presented at the Biennial Meeting of the Society for Research in Child Development (Symposium on symbolic play, A. Göncü, chair)*. Baltimore, Maryland: Elsevier Inc. https://doi.org/https://doi.org/10.1016/0273-2297(89)90036-1

Ekiru, S. (2018). Uadilishaji wa Mtoto katika Ujenzi wa Jamii Adili: Tathmini ya Hadithi za Watoto. *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo Yake*, 26 - 40.

Environments Inc. (2003). Pretend Play: A Staff Training Aid. *A Publication of the Environments Professional Group*, 15, 171 - 190.

Fein, G. (1989). Mind, Meaning and Affect: Proposals for a Theory of Pretence. *Developmental Review*, 9, 345 - 363.

Freud, S. (1920). *A General Introduction to Pschoanalysis*: PDF BooksWorld.

Gosso, Y., & Carvalho, A. M. A. (2013). Play and Cultural Context. In

*Encyclopedia on Early Childhood Development*, Universidade de São Paulo, Brazil, 1 - 7.

Mahan, R.A. (1969). Childhood Dependency and Parental Acceptance of Caretaking Roles., (Unpublished PhD Disertation), Iowa State University.

Maslow, A. H. (1943). A Theory of Human Motivation. *Psychological Review*, 50 (4), 370 - 396.

Matundura, E., Kobia, J., & Mukuthuria, M. (2013). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. *Mulika*, 32, 29 - 47.

Mosha. D. F. (2018). Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za watoto kwa watoto. *Mulika*, 37, 87 - 105.

Mushengezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Makerere University Press.

Ndossa, S. (2019, Machi 25). Ukali Siyo Njia Pekee ya Malezi (Chapisho la Mtandaoni). Limesomwa katika islamicftz. org/jamii-na-malezi/malezi/ukali-siyo-njia-pekee-ya-malezi/ (11/5/2020).

Ngugi, P. M. Y. (2015). Mbinu na Mikakati ya Kutumia Fasihi ya Watoto kama Bibliotherapia. *Kioo cha Lugha*, 13, 1 - 12.

Ngugi, P. M. Y., Lyimo, E.B., & Bakize, L. H. (2019). *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: TUKI.

Nespeca, S. M., & Reeve, J. B. (2003). *Picture Books Plus 100 Extension Activities in Art, Drama, Music, Math and Science.* Chicago, American Library Association.

Ojiambo, B. T. (2004). *Uhakiki wa Tamthilia ya Watoto kama Zao la Michezo ya Utotoni*. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Piaget, J. (1953). *The Origin of Intelligence in the Child*. New York: International Universities press, Inc.

Sheridan, M. (2002). *Play in Early Childhood: From Birth to Six Years*. London: Routledge.

Singer, D., & Singer, J. (2005). *Imagination and Play in the Electronic Age*. Cambridge: Harvard University Press.

Shima, G. (2012). Nafasi ya Vielelezo katika Fasihi ya Watoto (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walton, K. (1990). *Mimesis as Make-Believe: On the Foundations of the Representational Arts*. London: Harvard University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (2014, Mei 23). Wizara Yakemea Mtoto Kufungiwa Ndani ya Kasha Miaka Minne. Imesomwa katika tanzaniazalendo.org/zalendo/462/ (11/5/2020).